Iliwabidi walimu wafarague na kuongeza ubunifu wao ili kukamilisha mitaala ya masomo katika muda mfupi kuliko ule ulioratibiwa na wakuzaji mitaala. Mathalani, vipindi vilianza mapema kuliko kawaida yake na kuendelea hadi kupita saa kumi jioni na kuzima michezo ya baada ya madarasa. Mwalimu Bidii hakuwa na budi ila kujitoma ndani ya kinyang'anyiro hiki kwa vile hakupenda kuachwa nyuma. Hii ndiyo sababu ilimfanya kurauka kila siku. Lakini leo matarajio yake ya kuwahi kipindi cha saa kumi na mbili alfajiri yanaelekea kuyeyuka na kutokomea mithili ya theluji inavyoyeyuka na kugeuka kuwa maji yanayateremka kutoka milimani kufaidi walio mabondeni na kuviacha vileleta vya milima na kiu. Usiku uliopita ilikunya kidindia ungedhani ilikuwa mashindanoni. Barabara iliyotamani kutiwa sakafu tangu nchi ijinyakulie uhuru hadi sasa ikanyonya, ikameza na kutapika maji yakaloa kote. Wajuao chuku ya lugha walisema kilichozaliwa barabarani kilikuwa mama ya tope wala sio tope tu. Tazamo hili lilikejeli ile pikipiki aina ya 'Honda' aliyokuwa ameitumia Mwalimu Bidii kwa miongo miwili u nusu sasa – pikipiki aliyonunua baada ya kuomba mkopo kutoka kwenye chama cha ushirika cha akiba na mikopo baada ya miaka mitatu ya ajira. Ilimchukua miaka mitano kulipia mkopo wake.

Ilikuwa dhahiri tangu aiguse barabara hii kwamba alikuwa anajenga nyumba ya karata. Utelezi wa barabarani uliongezwa na magurudumu yaliyolika meno na kubwagwa chini halikuwa tukio lililokuwa ng'ambo ya utendekaji kamwe. Mara mojamoja ilimbidi Mwalimu Bidii kusalimu amri. Si hoja kwamba hakupiga hatua za maana kupunguza kitalifa cha kilomita kumi baina ya shule na nyumba yake ya kukodisha. Muda huu wote manyunyu ya mvua yalikuwa yanaendelea kudondoka ni kama yalikuwa na kinyongo na mzalendo huyu **aliyejitolea sabili** kuhudumia nchi yake. Alizidi kupambana akihema kama punda aliyebandikwa mzigo uliozidi uwezo wake akijaribu kuelekeza chombo chake **kisiende pewa** topeni. Kwa kweli hakuenda popote heri ule mfano wa simulizi ya Sofokile kumhusu mbingirisha mwamba kuupandisha kwenye mlima ulioteleza. Ingawa alishindwa kuukwea mlima, angaa angerudi nyuma sio kama mwalimu. Mwalimu alisakamwa kabisa; mbele na nyuma hakukuendeka!

Mbele yake kidogo alimwona mtu aliyemjua akiwa amevua viatu na kuvishika mikononi ili alikabili tope barabarani. Huyu alikuwa afisa wa maabara kwenye Zahanati ya Nafuu iliyokuwa karibu na Shule ya Mwera. Muala Mutia alipambana na hali yake bila kutazama nyuma aone dhiki alizokuwa anapitia mwalimu. Aliogopa kuchelewa kupokezwa zamu na mwenzake aliyehudumu usiku huo. Hakupenda nuksani za asubuhi ambazo Kechi angemzulia lau angechelewa hata kwa dakika chache tu. Kechi alikuwa mbali sana na ungwana na wenzake kazini waliepuka kumkorofisha kwani hakuna neno ambalo ulimi wake haungelitaja faraghani na hadharani. **Hakuwa na kaba ya ulimi**. Kama alikuwa na marafiki, achana na wandani, hawakujulikana pale zahanatini. Mutia aliambaa shari ili imwambae. Lakini leo ilikuwa muhali kwani hangeweza kukamilisha umbali wa kilomita tisa kwa miguu katika nusu saa iliyosalia kabla ya muda wa kupokezwa zamu. Na hakika lisilo budi mja muungwana hupatana nalo wala hapingani nalo.

Hatua kadhaa mbele yake alimpata yule mchuuzi anayewasambazia maziwa zahanatini amebwagwa chini na pikipiki yake na mitungi ikafunguka na kurembesha barabara kwa maziwa yaliyokuwamo. Kiplimo, jamaa aliyestawisha kilimo cha ufugaji katika Kijiji cha Kaplel, leo ameambulia hasara. Atarejea nyumbani mikono mitupu. Alisakama pale matopeni hadi Mutia alipomfikia na kuinua pikipiki iliyokuwa imeumbana mguu wake wa kulia asitoke.

"Hawa viongozi wetu wanahujumu maendeleo yetu kabisa! Mbona miaka hii yote barabara hii haijabandikwa lami?" Kiplimo akamaka baada ya kusimama.

Mutia akamkumbusha, "Lakini si ni nyinyi mna mazoea ya kukubali visenti vichache wakati wa uchaguzi ili kuwachagua wanafiki hawa? Kisha kuna wengine ambao husema 'Tunachagua mtu wetu', 'mtu wetu' ambaye sasa hana mwao kuhusu kero tunazopitia! Na wengine kama yule jirani yetu upande wa kusini haendi kupiga kura akidai kuwa kura yake moja haiwezi kuleta tofauti yoyote. Ni janga tumelichuma wakati wa uchaguzi sasa tuvumilie kulila. Wajua tangu kale, mwiba wa kujidunga huambiwi pole."

Mwalimu Bidii naye, baada ya kughairi nia, alikuwa ameegesha 'Honda' yake kando ya kigingi cha ua uliozingira shamba la yule mkwasi ambaye wengi hawakumjua ila walimsikia tu, akawa anamfuata Mutia akitumainia usaidizi wake. Alipowakaribia na kusikia malumbano yao, akatupa nukuu aliyowahi kuisikia kwa mtu asiyemkumbuka, "*Choices have consequences*!" Wale wawili wakaitikia kama ngonjera, "Ni kweli mwalimu!"

**Maswali**

a) Mikakati ya kukamilisha mitaala ya masomo iliwaathiri washikadau kwa namna mbalimbali. Taja athari **tatu** kwa wanafunzi. (alama 3)

……………………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………………….

FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

…………………………………………………………………………………………………….

b) Orodhesha changamoto **nne** zinazowatanza wahusika katika kutekeleza shughuli zao katika makala haya. (alama 4)

……………………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………………..

c) Thibitisha ukweli wa kauli kwamba 'uamuzi una athari zake' kwa kurejelea matukio **matatu** kuwahusu wananchi kama inavyosimuliwa katika kifungu hiki. (alama 3)

…………………………………………………………………………………………………….

…………………………………………………………………………………………………….

…………………………………………………………………………………………………….

d) Nakili kisawe cha '**bughudha**' kutoka kifunguni. (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………….

e) Andika visawe vya nahau zifuatazo: (alama 2)

(i) aliyejitolea sabili ……………………………………………………………………………

(ii) kisiende pewa ………………………………………………………………………………

f) (i) Bila kukanusha, eleza maana ya '**Hakuwa na kaba ya ulimi.'** (alama 1)

……………………………………………………………………………………………………..

g) Andika methali moja inayoasa kuhusu ulimi. (alama 1)

………………………………………………………………………………………………………

**2. Ufupisho** **(Alama 15)**

**Fupisha kifungu hiki kulingana maagizo yanayotolewa mwishoni mwake.**

Katika karne ya kumi na tisa bara la Afrika lilivamiwa na nchi za Ulaya kama vile Uingereza, Ufaransa, Ujerumani, Ubelgiji, Italia, Ureno na kadhalika na kutwaliwa. Uingiliaji huu haukuhusu Afrika pekee bali mataifa mengine katika ule ulioitwa ulimwengu usiostaarabika kama India. Kwa mujibu wa wanahistoria, Uingereza ndilo taifa lililojitwalia idadi kubwa ya nchi za ulimwengu chini ya mfumo wa kiutawala ulioitwa ukoloni labda kwa sababu kwamba Uingereza ni taifa lililokuwa limefikia ustawi mkubwa katika Ulaya nzima wakati huo. Bila shaka huu ulikuwa muktadha uliostahili matumizi ya usemi kuwa mwenye nguvu hupishwa na mataifa mengine ya Ulaya hayakuwa na budi ila kuipisha Uingereza ijilimbikizie mataifa ya ulimwengu na kuyaweka chini ya kwapa zake. Jambo lingine lililoiwezesha Uingereza kuyapiku mataifa mengine ya Ulaya katika kujipakulia koloni ulimwenguni ni kwamba Waingereza walitakadamu katika uvumbuzi wa vyombo vya usafiri wa majini na kwa hivyo waliweza kuzuru nchi za ulimwengu kwa wepesi zaidi na katika kipindi kifupi. Licha ya Uingereza kuwa katika nafasi bora ya kutwaa koloni ulimwenguni, mataifa mengine ya Ulaya hayakusubiri kugawiwa bali hayo pia yaling'ang'ania kumega sehemu fulani ya koloni. Huu mng'ang'anio ulikuwa kinyang'anyiro halisi ambacho kilimithilishwa na watu wanaogawana kipande cha mkate au nyama; kila mmoja akijikatia kadiri ya uwezo wake na makali ya kisu chake.

Uvamizi huu ulidhihirika kupitia utwaliwaji wa mamlaka ya kiutawala katika mataifa yaliyoathiriwa na kuwekwa chini ya himaya ya taifa husika kutoka Ulaya. Mtindo huu ulikinzana na tawala asilia za jamii mbalimbali za Kiafrika zilizokuwa na falme zao ambazo zilisambaratishwa baada ya kuangikwa kwa bendera ya taifa husika kutoka Ulaya. Hakukuwa na fursa ya kutathmini namna kila jamii katika kila eneo ilivyoendesha serikali yake chini ya viongozi wao mbalimbali. Usishangae kusikia kwamba Wazungu wengi waliipuuzilia mbali hii mifumo ya kiutawala au hata kudai kwamba wenyeji hawakuwa na mfumo wowote wa kujitawala. Uhasama uliokuwepo baina ya jamii tofauti pamoja na upekee wa mila na tamaduni zao zingine, ni mambo yaliyoangaziwa kwa kurunzi kali zaidi na kupuuza ukweli kwamba Waafrika walikuwa na mifumo mbalimbali ya kujiongoza.

Bara la Afrika lilikatwakatwa katika vipande mbalimbali na kugawiwa mataifa tofautitofauti ya Ulaya. Walibuni mipaka kiholela na kuwatenganisha watu wa jamii moja wakajipata kwenye

FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

nchi mbili tofauti. Si ajabu kwamba hata katika visa vya kidhalimu watu wa familia moja walitenganishwa kwa kuwekwa katika nchi mbili tofauti. Aidha, hata watu wa ukoo mmoja walitawanywa kimakusudi na kupelekwa katika maeneo mengine ya kijiografia yaliyoitwa nchi. Kadhalika, hata kuna maboma ambayo yalipigwa mpaka katikati na kumega sehemu moja kuitupa katika nchi tofauti na nyingine. Na kwa kweli asiyekujua hakudhamini. Watu walioathirika na tendo hili la kiholela waliona ugumu mkubwa kutii mipaka ya aina hii na kunao waliokaidi mipaka na kuendelea kutagusana na kutangamana na jamaa zao kokote walikopelekwa.

Tahakiki za wanahistoria hudai kwamba uvamizi wa Wazungu katika bara la Afrika, kwa kiwango cha juu zaidi ulileta na msukumo wa kutaka kunyakua maliasili kochokocho iliyojaa katika maeneo mengi. Madini kama chuma, makaa, shaba, almasi, dhahabu na mengine mengi yalijaa tele na viwanda vilivyokuwa vimestawishwa kutokana na Mageuzi ya Kiwanda ya Karne ya 19 vilihitaji mali ghafi na madini kwa wingi. Afrika illikuwa na hazina ya hiyo mali ghafi na ilifaa kutwaliwa bila pingamizi. Njia ya pekee ya kujihakikishia kuwepo mfululizo kwa bidhaa hii ilikuwa kuziweka nchi hizi chini ya himaya za serikali zao za Ulaya. Sina shaka walielewa msemo kwamba pavumapo palilie nao wageni wavamizi iliwabidi walilie bara lenye maliasili nyingi sana.

Licha ya majilio ya Wazungu barani Afrika kuangaziwa kwa uhasi, ni kweli kwamba kuna mambo mengi mazuri ambayo hayangetokea lau hawangalikuja. Ustawishaji wa miundomsingi, hasa njia, uliwezesha maeneo ya ndani kufikiwa bila bughudha nyingi. Ikumbukwe kwamba njia ya reli ya Kenya – Uganda, iliyojengwa mwanzoni mwa karne ya ishirini ilirahisisha kufanywa kwa shughuli katika maeneo ya ndani ya nchi. Kuna taasisi za matibabu, shule na vyuo vya mafunzo anuai katika taaluma mbalimbali vilivyojengwa na wakoloni. Hata viongozi wa kwanza baada ya nchi hizi kurejeshewa utawala wao, walisomea kwenye taasisi hizi. Mgala muue na haki yake mpe kwani ni stahili yake.

**Maswali**

a) Kwa maneno kati ya 80 – 90, andika hoja muhimu katika **aya mbili za kwanza**. (alama 8)

**Matayarisho**

…………………………………………………………………………………………………...

…………………………………………………………………………………………………...

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………….....

**Nakala safi**

……………………………………………………………………………………………...

……………………………………………………………………………………………...

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………….....

b) Fupisha aya za **tatu, nne** na **tano** ukizingatia athari hasi za ukoloni, kichocheo cha chake na manufaa ya ukoloni barani Afrika. (maneno 50) (alama 6)

**Matayarisho**

……………………………………………………………………………………………….....

……………………………………………………………………………………………...

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

**Nakala safi**

………………………………………………………………………………………………...

………………………………………………………………………………………………...

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

**3. Matumizi ya Lugha** **(Alama 40)**

a) Andika maneno yenye vitamkwa vya sifa zifuatazo: (alama 2)

(i) kikwamizwa sighuna cha kaakaa gumu, irabu ya nyuma juu, kikwamizwa ghuna cha kaakaa laini, irabu ya nyuma juu, kilainisho na irabu ya mbele juu

…………………………………………………………………………………………….

(ii) nazali ya midomoni, irabu ya mbele kati, nazali ya menoni na irabu ya nyuma wastani

..………………………………………………………………………………………….

FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

b) Taja sifa zinazoonyesha usawa baina ya kila jozi ya sauti hizi. (alama 1)

(i) /m/ na /w/ ……………………………………………………………………………………

(ii) /t/ na /ch/ ……………………………………………………………………………………

c) Eleza maana **mbili** zilizo katika sentensi: (alama 2)

Usijadili mtihani unaoendelea wakati huu.

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

d) Tumia wingi kuandika sentensi zifuatazo.

(i) Mkulima alilima ucheu ili kujiandaa kwa msimu wa upanzi wa nafaka. (alama 2)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

(ii) Shauri lake liliniepusha na janga la uwele hatari unaosambaa haraka. (alama 2)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

e) Onyesha katika sentensi **moja** matumizi **mawili** ya ritifaa (‘) katika lugha. (alama 2)

……………………………………………………………………………………………………

f) Zingatia maagizo katika mabano mwishoni mwa kila sentensi kuziandika upya.

(i) Wangia alipata mafunzo murua chuoni. Wangia ni stadi katika Kifaransa.

(Unganisha ukianzia: Mafunzo…) (alama 2)

………………………………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………….

(ii) Sherehe nyingi zilifanywa ili kuadhimisha ushindi wa Pute. (Tumia vitenzijina badala ya maneno yaliyopigiwa mistari.) (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(iii) Mari alinunua simutamba mpya kwa shilingi elfu kumi na kumtunza mwanafunzi bora.

(Anza na shamirisho ala.) (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

g) Ainisha mofimu katika maneno yafuatayo:

(i) katika (kitenzi) …………………………………………………………………... (alama 1)

(ii) achaguliwaye ……………………………………………………………………… (alama 2)

h) Tunga mfano **mojamoja** wa sentensi kwa kila muundo.

(i) S - KN (Ө)+KT(Ts+T+H+N) (alama 1)

………………………………………………………………………………………………….

(ii) S - KN (W+V)+KT(t+N+V) (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………..

i) Bainisha kiima, kiarifu na chagizo katika sentensi hii. (alama 3)

Mhandisi shupavu atakagua ujenzi wa ghorofa hatua kwa hatua.

…………………………………………………………………………………………………..

j) Eleza matumizi ya kiambishi **-o** katika sentensi ifuatayo: (alama 1)

Waliofanikiwa walifanya makadirio mazuri.

……………………………………………………………………………………………………

k) Tambua kisha ainisha nomino katika sentensi hii: (alama 2)

Mashabiki wengi walipiga vigelegele Kocha Manoa alipotaja kikosi cha wachezaji wake.

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

l) Vishazi tegemezi vina dhima za kivumishi na kielezi. Tunga sentensi **mojamoja** kuonyesha kila dhima. (alama 2)

(i) kivumishi: ……………………………………………………………………………………..

(ii) kielezi: ………………………………………………………………………………………..

m) Onyesha maana **mbili** za neno '**bunda**' kwa kutungia sentensi **mbili** tofauti. (alama 2)

(i) ………………………………………………………………………………………………

(ii) ………………………………………………………………………………………………

n) Kwa kutumia sentensi **moja**, onyesha miundo **miwili** ya virai husishi. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………….

FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

o) Akifisha.

siku ya kiswahili duniani iliadhimishwa na wengi ilifana (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

p) Jaza mapengo kwa maneno yanayostahili. (alama 1)

Kinza ni kwa pinga na tambua ni kwa …………………………….. ilhali nata ni kwa ……………………………….

r) Onyesha katika sentensi maana ya nahau: '**shika shokoa**'. (alama 1)

………………………………………………………………………………………………..

s) Kasura aligundua kwamba Ogina alikuwa na uwezo mwingi wa kukabili Somo la Hisabati na akaamua kwenda mara kwa mara kupewa ushauri na Ogina hata akaimarika. Taja methali inayoweza kutumiwa kuafiki muktadha wa Karusa. (alama 1)

……………………………………………………………………………………………….

t) Kwa kuzingatia maana, sentensi ifuatayo inaweza kuwa katika **aina mbili**. Zitaje. (alama 1)

Mkiondoka wawiliwawili, mtafika haraka.

(i) ……………………………………………………………………………………………

FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

(ii) ……………………………………………………………………………………………….

**4. Isimujamii** **(Alama 10)**

a) Eleza sifa **tano** za lugha ambayo wewe kama mnyapara wa kiwanda cha kusaga miwa cha Kimatuni utatumia ukiwahutubia wafanyakazi walio chini yako. (alama 5)

………………………………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………….

b) *Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.* (alama 5)

"Polepole, Mama Mercy! Unajua si kupenda kwangu. Tena si hali itakayodumu milele. Baada ya siku chache tu, tutakuwa tumekamilisha mradi huo wenye dharura. Kisha tutakuwa na muda wa kila kitu. Hili, Mama Mercy, ni kile tunaita *bad coincidence*… nimebanwa na kazi. Unanielewa …?

"Dadii…njaa…sana!"

Fafanua sifa **tano** za lugha inayotumika katika huu muktadha wa familia. (alama 5)

……………………………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………….

FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

JINA……………………………..........................................................NAMBARI …………..……………………

SHULE ………………………………………………………….………………………......INDEX...................................

TAREHE ………………….……..........SAHIHI..............................LENGO.......................................

**102/2**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 2**
**MUDA: SAA 1¾**

# SERIES 5 2023 MOCK

## KIDATO CHA NNE

*Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari Kenya. (K.C.S.E)*

**KISWAHILI**
**KARATASI YA PILI**
**102/2**
**MUDA: SAA 1¾**

**Maagizo**

h) *Andika jina na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

i) *Jibu maswali yote.*

j) *Majibu yaandikwe katika nafasiulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*

k) *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

l) *Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.*

**KWA MATUMIZI YA MITAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| JUMLA | 80 | |

FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

1. **SEHEMU YA A: HAMU YA HAMO**

Hamo alirauka majogoo kuanza maandalizi ya mapema. Hakutaka kukosa sherehe ya sikukuuu ya Jamhuri kama alivyokuwa amekosa ile ya mashujaa. Siku hiyo alipofika kwenye lango kuu la uga ambako sherehe zilitendeka, askari mmoja mwenye kofia nyekundu, miwani myeusi na bunduki kifuani alimnyoshea kidole na kumwambia, “Kwenda nyumbani kijana . Unafika hapa baada ya rais kuingia kwani wewe ni rais wa Marekani?” swali hilo lilimsumbua kwa siku kadhaa, akawachukia maafisaa wa usalama, na likamtwanga kwa nguvu sana asubuhi ya Jamuhuri. Alimaliza maandalizi na kupiga milundi uwanjani.

“Una kitambulisho?” Hamo aliona ajibu kwa kukitoa na wakati huu afisaa wa usalama alimruhusu aingie bila maswali zaidi. “Huyu amechoka sana. Hata sare yake ya bluu imechujuka jamani!” Hamo alijiambia akiingia uwanjani. Uwanja ulikula watu bila kushiba, kwani kulikuwa na mapengo ya hapa na pale kama kinywa kilichong’oka meno. Bw. Hamo alitafuta nafasi karibu na jukwaa lakini katika sehemu iliyotengwa “wananchi wa kawaida.” Hayo maneno matatu yalikuwa yamemsumbua Hamo akijiuliza mbona wale wengine walijiona wasiokuwa wa kawaida. Hata, hivyo, hakutaka fikra hizo ziboronge hamu yake ya siku.

Basi, bendi ya wanajeshi ilisikika na kiongozi wao akawa na fimbo fulani aliyoizungusha mkononi hapa na pale na wakati mwingine kuirusha juu, akakimbi kuidaka kabla ya kugusa ardhini. Vikosi vitatu vya wanajeshi waliovalia sare za rangi tatu tofauti: nyekundu, bluu na nyeupe viliingia kwa kupendeza. Kila mwanajeshi alikuwa ameishika bunduki yake kwa mkono wa kulia, na kuurusha mkono wa kushoto mbele na nyuma kana kwamba hawakupendezwa na mikono yao, ila mikono hiyo ilirushwa kwa pamoja na kuunda safu nzuri, ungedhani mikono hiyo iliunganishwa na kufungwa. Kiongozi mmoja aliyekuwa na kitara mkononi alisimama katikati na kupaaza sauti kubwa ilyosikika kanakwamba alikuwa na kipaza sauti. Kwa pamoja wanajeshi waliichapa miguu yao chini kwa nguvu kana kwamba wakimuua nyoka na kutulia tuli! Haya yalimshangaza Hamo kwani alisikia ni kama kiongozi alilia “Hooooo ho!

Muda ulizidi kuyoyoma na punde si punde rais aliingia kwenye gari lililompa uwezo wa kuwasalimu wananchi. Bw. Hamo alipiga kelele kama wananchi wengine na rais alipopita karibu naye, Bw. Hamo alimwambia “Nakupenda rais!” Rais alitabasamu na kuangalia upande huo huku akiweka viganja vyake pamoja na kuinua juu, ishara ya kwamba, “tu pamoja” , jambo lililomfurahisha Hamo aliyetabasamu nusura aonyeshe magego yake. Burudani iliendelea pale na wanajeshi wakapendeza kwa vioja na viroja vyao; mara waangalie mbele, mara wapinduke ghafla kama walioumwa na siafu, mara wasukumane mikono na kujipanga vizuri zaidi, mara wawe wawili wawili, waunde ruwaza za kupendeza; haya yote baada ya kilio cha yule kiongozi ambacho Hamo hakusikia kikibadilika pahubwa, kwani kilicheza “Hooooho” na maneno mengine ambayo Hamo aliamini kuwa hayakuwa kwa mojawapo ya lugha alizozielewa.

Kilele cha siku kilikuwa hotuba ndefu ya rais ya Kiingereza na japo Hamo hakung’amua chochote, alihisi kuwa ilikuwa siku iliyofana, na kwa kuwa rais alimjibu salamu zake kwa heshima kubwa, alijiona kuwa shujaa. Muhimu zaidi alikula yamini kuwa mwanajesi, ambaye ama awe Yule wa “hooooooho!” au Yule wa kurusha na kudaka fimbo kabla ifike ardhini.

**MASWALI**

a) Mbona Hamo aliamka wakati wa majogoo (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………b) Tofautisha maafisa wawili waliotajwa kwenye kifungu kihulka. (alama 4)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………c) Eleza sifa tatu za rais kulingana na taarifa. (alama 3)

FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………d) Mbona Homa alikuwa yamini kuwa mwanajesi. (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………………e) Thibitisha suala la utabaka kwa kurejelea kifungo. (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………………

f) Toa mfano mmoja wa matumizi ya mbinu ya mbinu ya uhuishaji kutoka kwenye kifungo.

(alama 1)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………g) Eleza maana ya maneno haya kulingana na taarifa: (alama 3)

i) uga

…………………………………………………………………………………………………………

ii) boronga

…………………………………………………………………………………………………………iii) kula yamini

…………………………………………………………………………………………………………

**2. <u>UFUPISHO</u>**

*Soma kifungo kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.*

Mirundiko ya taka pamoja na utaratibu usiofaa wa uzoaji wake ni tisho kubwa kwa siha ya umma pamoja na mazingira . Hii ni kwa kuwa taka huwa ni makaazi ya wadudu na wanyama waharibifu kama nzi, mbu, kombamwiko na panya ambao hueneza magonjwa na kuharibu vitu vyenye dhamani. Maji taka nayo, pamoja na mifuko ya sandarusi huwa mastakimu ya wadudu na virusi vinavyoleta magonjwa mbalimbali.

Mifuko ya sandarusi ina madhara kwa kuwa huziba mitaro ya maji na kuzuia upitaji wa maji. Madhara hutokeza wakati wa mvua za ngarika. Maji haya husababisha mafuriko ambayo huleta hasara ya mali na wakati mwingine ya uhai. Fauka ya haya, mifuko hii huwasakama tumboni wanyama sio wa nyumbani tu, bali wa porini na majini.

Kwa sababu ya hatari zitokanazo na taka, pana haja kutafuta njia na teknolojia ya kwanza kukabiliana na tatizo hili ili kuyatunza mazingira na siha ya umma. Njia mojawapo ya kufanya hivi ni kuelimisha na kuhimiza umma kuwa na uangalifu katika matumizi ya bidhaa na raslimali ili kupunguza uzalishaji wa taka. Matumizi ya bidhaa kwa njia ya ubadhirifu huwa chanzo cha uzalishaji wa taka kwa wingi. Kwa mfano, maji ni raslimali ambayo imeendelea kutumiwa kwa ubadhirifu na hiyo uzalishaji maji taka kwa wingi. Raslimali hii inaweza ikatumiwa kwa njia endelevu. Kwa mfano, badala ya kutumia bafu ya nyumbani kuoga mtu anaweza kutumia maji ya karai.

Watu wengi huchukulia taka kuwa kitu kisicho na manufaa yoyote. Hawajui kuwa kwa kutumia teknolojia endelezi, taka nyingi zinaweza zikageuzwa na kuwa na manufaa mengi. Vijana wadogo sehemu za mashambani wanahitaji pongezi kwa kuwa na utambuzi huu. Wengi, kwa kukosa hela za kununulia mipira ya viwandani, hutumia teknolojia endelezi ambapo taka hugeuzwa na kuwa na manufaa.

Baadhi ya wananchi wenye ubunifu nao wameanzisha miradi ya kuzoa takataka kutoka majumbani mwa watu kwa ada kisha huzipeleka taka hizi kule zitakakobadilishwa ili ziwe na manufaa. Mifuko na mabaki ya sandarusi hupelekwa katika viwanda vinavyotengeneza bidhaa za plastiki kama matangi, mitungi, sapatu na champali. Taka hizi huwa malighafi ya kutengeneza bidhaa nungine.

Taka za chupa na chuma nazo huuzwa katika viwanda vinavyozigeuza kuwa na manufaa tena. Taka za karatasi hutumiwa kutengeneza bidhaa kama vitabu, katoni, shashi za chooni na magazeti.

FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM **0729125181**

Taka zinaweza pia kugeuzwa kuwa zenye faida kwa kuzitumia kufanyia mboji. Ni muhimu kutambua kuwa si kila aina ya taka inaweza kutumiwa hapa. Taka zinazoweza kufanyiwa mboji ni zile ambazo huoza kwa haraka, kama vile: mabaki ya vyakula mboga na matunda. Kwa sadfa, hizi ndizo taka zinazozalishwa zaidi siku na hasa sehemu za mjini katika maeneo ya biashara kama mikahawa na hospitali. Mtu akiwa na nafasi anaweza kuchimba shimo ambalo atafukia taka ili kutengeneza mbolea. Hii ni njia isiyodhuru mazingira na yenye manufaa kemkem. Kwanza, kugeuza taka ambayo inaweza kuwa hatari na kuifanya iwe yenye manufaa. Kwa hivyo hutatua matatizo ya kiafya yanayoweza kutokana na mirundiko ya taka. Mchanga nao hufaidika kupata virutubishi. Mbolea kama hii inaweza ikatumika kukuzia mboga au maua katia bustani. Maji taka, hasa yanayotumika kuosha vyombo, nayo yanaweza kutumika kunyunyizia mashamba madogo ya mboga au bustani za maua. Maji taka haya yanahitaji kutayarishwa njia mahususi ya kuyaelekeza katika mashamba haya baada ya kutumiwa. Anglalabu watu wengi wana mazoea ya kuchoma taka. Ni kawaida kupata matanuri ya kuchomea taka katika baadhi ya mitaa, shule na hospitali. Badala ya kupoteza moto huu bure bilashi, inawezekana pakawekwa birika kubwa au tangi la chuma ambalo litatuma moto huo kuchemsha maji. Maji haya yanaweza yakatumiwa katika shughuli za nyumbani.

Hata hivyo ni muhimu kukumbuka kuwa kuna baadhi ya taka ambazo ni hatari na huenda zisigeuzwe ili kutumika kwa njia yenye faida. Taka hizi ni kama vile mikebe au vifaa vingine vyenye kubeba sumu au dawa hatari. Ni bora kuvitupa vifaa hivi katika mashimo marefu au vyoo vya mashimo.

Kwa vyovyote vile, si jambo muhali kwa watu popote wanapoishi kulinda siha yao pamoja na kutunza mazingira. Ulinzi na utunzaji huo huhitaji uangalifu mkubwa katika utupaji taka.

a) Fupisha ujumbe wa aya tatu za kwanza kwa maneno 100. (alama 8, 1 utiririko)

**Matayarisho**

………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………

**Nakala safi**

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………b) Kwa kurejelea

aya ya tano hadi ya tisa, onyesha manufaa ya taka (maneno 80)

(alama 7, 1 utiririko)

**Matayarisho**

………………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………

**Nakala safi**

………………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………………

FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM **0729125181**

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

3. **MATUMIZI YA LUGHA**

a) Unda maneno yenye muundo wa sauti zifuatazo: (alama 2)

i) King'ong'o cha kaakaa laini, irabu ya nyuma wastani, irabu ya chini kati.

………………………………………………………………………………………………

ii) Kikwamizo hafifu cha koromeo, irabu ya nyuma juu , kiyeyusho cha kaakaa gumu, irabu ya nyuma kati

………………………………………………………………………………………………

b) Andika neno moja lenye silabi za muundo ufuatao. (alama 1)

irabu, konsonantii +konsonanti, irabu+konsonanti, irabu

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

c) Bainisha matumizi ya 'ki' katika sentensi ifuatayo: (alama 2)

Akiendelea kukichezea, kichuma chake ki motoni.

………………………………………………………………………………………………

d) Unda vitenzi kutokana na nomino zifuatazo (alama 2)

i) hasidi-

………………………………………………………………………………………………

ii) tafakuri-

………………………………………………………………………………………………

FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

e) Tunga sentensi yenye mpangilio wa maneno ufuatao: (alama 2)

nomino katika ngeli ya U-zi wingi.

Kivumishi cha pekee

Kitenzi halisi

Kielezi cha kiasi

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

f) Ainisha viambishi: (alama 2)

haujiki

……………………………………………………………………………………………………g) Tumia mzizi –ny- kukamiliisha sentensi hii (alama 1)

Miti ya msitu huo ime ………………………… mvua katika jimbo hili

……………………………………………………………………………………………………

h) Tumia mzizi '-ema' katika sentensi kama: (alama 3)

i) kivumishi

……………………………………………………………………………………………………

ii) kielezi

……………………………………………………………………………………………………

iii) nomino

……………………………………………………………………………………………………

i) Mchezaji alipoona kiyu* aliya gugumia maji

Kando na matumizi haya ya kinyota, taja matumizi mengine mawili ya kiakifishi hiki. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………j)Tunga sentensi ya swali ukitumia kiwakilishi nafsi ambata nafsi ya pili wingi (alama2)

………………………………………………………………………………………

k) Andika sentensi hii iwe katika usemi wa taarifa

“Nyinyi nyote mkipita nitawanunulia mikate miwili kesho jioni, mwalimu alituambia. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

l) Andika kinyume cha sentensi hii:

Tajiri wengi walikashifiwa baada ya kuhamia msituni (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………..

m) Ainisha shamirisho na chajizo: (alama 4)

Mwanamke mzee alipikiwa chai tamu kwa sufuria kubwa leo asubuhi na mjukuu wake.

n) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao: (alama 2)

$KN(\bar{S}\ ) + KT\big(t + KN_2\ (N + V)\big)$

…………………………………………………………………………………………………

o) Mohamed alifuzu mtihani huo vizuri kwa sababu alisoma kwa bidii (maliza kwa mtihani huo vizuri) (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………

p) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielezo cha matawi.

Lilikuwa limelimwa na wakulima hodari sana. (alama 4)

q) Andika ukubwa wingi wa sentensi hii

Mtoto alimuua nyoka mdogo kwa kumpiga kichwani (alama 1)

………………………………………………………………………………………………………

r) Ainisha virai vinne katika sentensi hii:

Vipya kabisa vilivyoagizwa jana sokoni vitanunuliwa na mtoto wa Juma (alama 2)

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

s) Tunga sentensi moja kionyesha maana mbili za neno 'funza' (alama 2)

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

t) Mkungu ni kwa ndizi, koja ni kwa …………….. na…………….. ni kwa mboga . (alama 1)

**4 ISIMUJAMII (ALAMA 10)**

a) Terry: Liandikwalo ndilo liwalo. "Since when has man ever changed his destiny?"

i) Tambua mtindo wa lugha uliotumiwa na mzungumzaji wa maneno haya. (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………

ii) Eleza sababu nne zinazopelekea wazungumzaji kutumia mtindo huu. (alama 4)

…………………………………………………………………………………………………

b) Wewe ni mfanyikazi katika kiwanda cha kutengeneza mavazi. Eleza sifa tano za lugha utayotumia unapowasiliana na wafanyakazi wenzako. (alama 5)

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

**JINA……………………………………………..NAMBARI YAUSAJILI…………..............**

**SCHOOL.........................................................................INDEX.............................................**

**TAREHE…………………….…SAHIHI..............………...…LENGO....................................**

**102/2**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 2**
**LUGHA**
**MUHULA WA II**
**MUDA : Saa 2 ½**

# SERIES 6 2023 MOCK

## KIDATO CHA NNE

**Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (K.C.S.E)**

**Maagizo**

*a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
*b) Tia sahihi yako na kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
*c) Jibu maswali yote.*
*d) Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
*e) Majibu yote ni lazima yaandikwe kwa lugha ya* ***Kiswahili.***

***Kwa matumizi ya Mtahini Pekee :***

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1. Ufahamu | 15 | |
| 2. Muhtasari | 15 | |
| 3. Matumizi ya Lugha | 40 | |
| 4. Isimu Jamii | 10 | |
| JUMLA | 80 | |

FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

***Karatasi hii ina kurasa 12 zilizopigwa chapa. Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.***

**1. Ufahamu** **(Alama 15)**

**Soma makala halafu ujibu maswali yanayofuatia.**

Leo Mwalimu Bidii amerauka kama ada yake kwa ajili ya kutekeleza wajibu wake kwa wanafunzi wake Shuleni Mwera. Anaelewa barabara kwamba mchapuko wa ghafla wa gonjwa la korona kule Uchina, ulitikisa na kuvuruga dunia nzima katika nyanja zote za maisha ya binadamu. Miongoni mwa nyanja zilizoathiriwa zaidi ni elimu ambayo huongoza nyanja zingine za maisha. Awali, taasisi zote za elimu zilifungwa kama hatua muhimu ya kudhibiti msambao wa uwele huu. Baadaye afueni ilipodhihiri, na ushauri kutolewa na wataalamu wa afya, mataifa mbalimbali yalibuni taratibu za kurejelewa kwa shughuli za masomo katika taasisi zote. Labda marejeleo haya hayakuwa na ugumu kama ilivyokuwa namna ya kufidia na kurejelewa kwa mfumo wa kawaida shuleni. Naam, mwiba uchomeapo ndipo utolewapo na tiba mjarabu ni ile itokayo kwa mwele mwenyewe. Wizara ya elimu nchini iliratibu mihula upya na kuvuruga mazoea. Hii ni hatua iliyowasababishia **bughudha** washikadau wote; sio walimu, wazazi, wauzaji na wanafunzi. Sijui mizani gani iliyotumiwa kupima, lakini watu wengi walihisi kwamba ni walimu waliokumbwa na usumbufu mkubwa zaidi.

Iliwabidi walimu wafarague na kuongeza ubunifu wao ili kukamilisha mitaala ya masomo katika muda mfupi kuliko ule ulioratibiwa na wakuzaji mitaala. Mathalani, vipindi vilianza mapema kuliko kawaida yake na kuendelea hadi kupita saa kumi jioni na kuzima michezo ya baada ya madarasa. Mwalimu Bidii hakuwa na budi ila kujitoma ndani ya kinyang'anyiro hiki kwa vile hakupenda kuachwa nyuma. Hii ndiyo sababu ilimfanya kurauka kila siku. Lakini leo matarajio yake ya kuwahi kipindi cha saa kumi na mbili alfajiri yanaelekea kuyeyuka na kutokomea mithili ya theluji inavyoyeyuka na kugeuka kuwa maji yanayateremka kutoka milimani kufaidi walio mabondeni na kuviacha vileleta vya milima na kiu. Usiku uliopita ilikunya kidindia ungedhani

ilikuwa mashindanoni. Barabara iliyotamani kutiwa sakafu tangu nchi ijinyakulie uhuru hadi sasa ikanyonya, ikameza na kutapika maji yakaloa kote. Wajuao chuku ya lugha walisema kilichozaliwa barabarani kilikuwa mama ya tope wala sio tope tu. Tazamo hili lilikejeli ile pikipiki aina ya 'Honda' aliyokuwa ameitumia Mwalimu Bidii kwa miongo miwili u nusu sasa – pikipiki aliyonunua baada ya kuomba mkopo kutoka kwenye chama cha ushirika cha akiba na mikopo baada ya miaka mitatu ya ajira. Ilimchukua miaka mitano kulipia mkopo wake.

Ilikuwa dhahiri tangu aiguse barabara hii kwamba alikuwa anajenga nyumba ya karata. Utelezi wa barabarani uliongezwa na magurudumu yaliyolika meno na kubwagwa chini halikuwa tukio lililokuwa ng'ambo ya utendekaji kamwe. Mara mojamoja ilimbidi Mwalimu Bidii kusalimu amri. Si hoja kwamba hakupiga hatua za maana kupunguza kitalifa cha kilomita kumi baina ya shule na nyumba yake ya kukodisha. Muda huu wote manyunyu ya mvua yalikuwa yanaendelea kudondoka ni kama yalikuwa na kinyongo na mzalendo huyu **aliyejitolea sabili** kuhudumia nchi yake. Alizidi kupambana akihema kama punda aliyebandikwa mzigo uliozidi uwezo wake akijaribu kuelekeza chombo chake **kisiende pewa** topeni. Kwa kweli hakuenda popote heri ule mfano wa simulizi ya Sofokile kumhusu mbingirisha mwamba kuupandisha kwenye mlima ulioteleza. Ingawa alishindwa kuukwea mlima, angaa angerudi nyuma sio kama mwalimu. Mwalimu alisakamwa kabisa; mbele na nyuma hakukuendeka!

Mbele yake kidogo alimwona mtu aliyemjua akiwa amevua viatu na kuvishika mikononi ili alikabili tope barabarani. Huyu alikuwa afisa wa maabara kwenye Zahanati ya Nafuu iliyokuwa karibu na Shule ya Mwera. Muala Mutia alipambana na hali yake bila kutazama nyuma aone dhiki alizokuwa anapitia mwalimu. Aliogopa kuchelewa kupokezwa zamu na mwenzake aliyehudumu usiku huo. Hakupenda nuksani za asubuhi ambazo Kechi angemzulia lau angechelewa hata kwa dakika chache tu. Kechi alikuwa mbali sana na ungwana na wenzake kazini waliepuka kumkorofisha kwani hakuna neno ambalo ulimi wake haungelitaja faraghani na hadharani. **Hakuwa na kaba ya ulimi**. Kama alikuwa na marafiki, achana na wandani, hawakujulikana pale zahanatini. Mutia aliambaa shari ili imwambae. Lakini leo ilikuwa muhali kwani hangeweza kukamilisha umbali wa kilomita tisa kwa miguu katika nusu saa iliyosalia kabla ya muda wa kupokezwa zamu. Na hakika lisilo budi mja muungwana hupatana nalo wala hapingani nalo.

Hatua kadhaa mbele yake alimpata yule mchuuzi anayewasambazia maziwa zahanatini amebwagwa chini na pikipiki yake na mitungi ikafunguka na kurembesha barabara kwa maziwa yaliyokuwamo. Kiplimo, jamaa aliyestawisha kilimo cha ufugaji katika Kijiji cha Kaplel, leo ameambulia hasara. Atarejea nyumbani mikono mitupu. Alisakama pale matopeni hadi Mutia alipomfikia na kuinua pikipiki iliyokuwa imeumbana mguu wake wa kulia asitoke.

"Hawa viongozi wetu wanahujumu maendeleo yetu kabisa! Mbona miaka hii yote barabara hii haijabandikwa lami?" Kiplimo akamaka baada ya kusimama.

Mutia akamkumbusha, "Lakini si ni nyinyi mna mazoea ya kukubali visenti vichache wakati wa uchaguzi ili kuwachagua wanafiki hawa? Kisha kuna wengine ambao husema 'Tunachagua mtu wetu', 'mtu wetu' ambaye sasa hana mwao kuhusu kero tunazopitia! Na wengine kama yule jirani yetu upande wa kusini haendi kupiga kura akidai kuwa kura yake moja haiwezi kuleta tofauti yoyote. Ni janga tumelichuma wakati wa uchaguzi sasa tuvumilie kulila. Wajua tangu kale, mwiba wa kujidunga huambiwi pole."

Mwalimu Bidii naye, baada ya kughairi nia, alikuwa ameegesha 'Honda' yake kando ya kigingi cha ua uliozingira shamba la yule mkwasi ambaye wengi hawakumjua ila walimsikia tu, akawa anamfuata Mutia akitumainia usaidizi wake. Alipowakaribia na kusikia malumbano yao, akatupa nukuu aliyowahi kuisikia kwa mtu asiyemkumbuka, "*Choices have consequences*!" Wale wawili wakaitikia kama ngonjera, "Ni kweli mwalimu!"

**Maswali**

a) Mikakati ya kukamilisha mitaala ya masomo iliwaathiri washikadau kwa namna mbalimbali. Taja athari **tatu** kwa wanafunzi. (alama 3)

…………………………………………………………………………………………………….

…………………………………………………………………………………………………….

…………………………………………………………………………………………………….

FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

b) Orodhesha changamoto **nne** zinazowatanza wahusika katika kutekeleza shughuli zao katika makala haya. (alama 4)

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

c) Thibitisha ukweli wa kauli kwamba 'uamuzi una athari zake' kwa kurejelea matukio **matatu** kuwahusu wananchi kama inavyosimuliwa katika kifungu hiki. (alama 3)

………………………………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………….

d) Nakili kisawe cha '**bughudha**' kutoka kifunguni. (alama 1)

………………………………………………………………………………………………….

e) Andika visawe vya nahau zifuatazo: (alama 2)

(i) aliyejitolea sabili ………………………………………………………………………………

(ii) kisiende pewa …………………………………………………………………………………

f) (i) Bila kukanusha, eleza maana ya '**Hakuwa na kaba ya ulimi.'** (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………..

g) Andika methali moja inayoasa kuhusu ulimi. (alama 1)

……………………………………………………………………………………………………

FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

**2. Ufupisho** **(Alama 15)**

**Fupisha kifungu hiki kulingana maagizo yanayotolewa mwishoni mwake.**

Katika karne ya kumi na tisa bara la Afrika lilivamiwa na nchi za Ulaya kama vile Uingereza, Ufaransa, Ujerumani, Ubelgiji, Italia, Ureno na kadhalika na kutwaliwa. Uingiliaji huu haukuhusu Afrika pekee bali mataifa mengine katika ule ulioitwa ulimwengu usiostaarabika kama India. Kwa mujibu wa wanahistoria, Uingereza ndilo taifa lililojitwalia idadi kubwa ya nchi za ulimwengu chini ya mfumo wa kiutawala ulioitwa ukoloni labda kwa sababu kwamba Uingereza ni taifa lililokuwa limefikia ustawi mkubwa katika Ulaya nzima wakati huo. Bila shaka huu ulikuwa muktadha uliostahili matumizi ya usemi kuwa mwenye nguvu hupishwa na mataifa mengine ya Ulaya hayakuwa na budi ila kuipisha Uingereza ijilimbikizie mataifa ya ulimwengu na kuyaweka chini ya kwapa zake. Jambo lingine lililoiwezesha Uingereza kuyapiku mataifa mengine ya Ulaya katika kujipakulia koloni ulimwenguni ni kwamba Waingereza walitakadamu katika uvumbuzi wa vyombo vya usafiri wa majini na kwa hivyo waliweza kuzuru nchi za ulimwengu kwa wepesi zaidi na katika kipindi kifupi. Licha ya Uingereza kuwa katika nafasi bora ya kutwaa koloni ulimwenguni, mataifa mengine ya Ulaya hayakusubiri kugawiwa bali hayo pia yaling’ang’ania kumega sehemu fulani ya koloni. Huu mng’ang’anio ulikuwa kinyang’anyiro halisi ambacho kilimithilishwa na watu wanaogawana kipande cha mkate au nyama; kila mmoja akijikatia kadiri ya uwezo wake na makali ya kisu chake.

Uvamizi huu ulidhihirika kupitia utwaliwaji wa mamlaka ya kiutawala katika mataifa yaliyoathiriwa na kuwekwa chini ya himaya ya taifa husika kutoka Ulaya. Mtindo huu ulikinzana na tawala asilia za jamii mbalimbali za Kiafrika zilizokuwa na falme zao ambazo zilisambaratishwa baada ya kuangikwa kwa bendera ya taifa husika kutoka Ulaya. Hakukuwa na fursa ya kutathmini namna kila jamii katika kila eneo ilivyoendesha serikali yake chini ya viongozi wao mbalimbali. Usishangae kusikia kwamba Wazungu wengi waliipuuzilia mbali hii mifumo ya kiutawala au hata kudai kwamba wenyeji hawakuwa na mfumo wowote wa kujitawala. Uhasama uliokuwepo baina ya jamii tofauti pamoja na upekee wa mila na tamaduni zao zingine, ni mambo yaliyoangaziwa kwa kurunzi kali zaidi na kupuuza ukweli kwamba Waafrika walikuwa na mifumo mbalimbali ya kujiongoza.

FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

Bara la Afrika lilikatwakatwa katika vipande mbalimbali na kugawiwa mataifa tofautitofauti ya Ulaya. Walibuni mipaka kiholela na kuwatenganisha watu wa jamii moja wakajipata kwenye nchi mbili tofauti. Si ajabu kwamba hata katika visa vya kidhalimu watu wa familia moja walitenganishwa kwa kuwekwa katika nchi mbili tofauti. Aidha, hata watu wa ukoo mmoja walitawanywa kimakusudi na kupelekwa katika maeneo mengine ya kijiografia yaliyoitwa nchi. Kadhalika, hata kuna maboma ambayo yalipigwa mpaka katikati na kumega sehemu moja kuitupa katika nchi tofauti na nyingine. Na kwa kweli asiyekujua hakudhamini. Watu walioathirika na tendo hili la kiholela waliona ugumu mkubwa kutii mipaka ya aina hii na kunao waliokaidi mipaka na kuendelea kutagusana na kutangamana na jamaa zao kokote walikopelekwa.

Tahakiki za wanahistoria hudai kwamba uvamizi wa Wazungu katika bara la Afrika, kwa kiwango cha juu zaidi uliletwa na msukumo wa kutaka kunyakua maliasili kochokocho iliyojaa katika maeneo mengi. Madini kama chuma, makaa, shaba, almasi, dhahabu na mengine mengi yalijaa tele na viwanda vilivyokuwa vimestawishwa kutokana na Mageuzi ya Kiwanda ya Karne ya 19 vilihitaji malighafi na madini kwa wingi. Afrika illikuwa na hazina ya hiyo malighafi na ilifaa kutwaliwa bila pingamizi. Njia ya pekee ya kujihakikishia kuwepo mfululizo kwa bidhaa hii ilikuwa kuziweka nchi hizi chini ya himaya za serikali zao za Ulaya. Sina shaka walielewa msemo kwamba pavumapo palilie nao wageni wavamizi iliwabidi walilie bara lenye maliasili nyingi sana.

Licha ya majilio ya Wazungu barani Afrika kuangaziwa kwa uhasi, ni kweli kwamba kuna mambo mengi mazuri ambayo hayangetokea lau hawangalikuja. Ustawishaji wa miundomsingi, hasa njia, uliwezesha maeneo ya ndani kufikiwa bila bughudha nyingi. Ikumbukwe kwamba njia ya reli ya Kenya – Uganda, iliyojengwa mwanzoni mwa karne ya ishirini ilirahisisha kufanywa kwa shughuli katika maeneo ya ndani ya nchi. Kuna taasisi za matibabu, shule na vyuo vya mafunzo anuai katika taaluma mbalimbali vilivyojengwa na wakoloni. Hata viongozi wa kwanza baada ya nchi hizi kurejeshewa utawala wao, walisomea kwenye taasisi hizi. Mgala muue na haki yake mpe kwani ni stahili yake.

**Maswali**

a) Kwa maneno kati ya 80 – 90, andika hoja muhimu katika **aya mbili za kwanza**. (alama 8)

**Matayarisho**

**Nakala safi**

FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM **0729125181**

b) Fupisha aya za **tatu, nne** na **tano** ukizingatia athari hasi za ukoloni, kichocheo cha chake na manufaa ya ukoloni barani Afrika. (maneno 50) (alama 6)

**Matayarisho**

…………………………………………………………………………………………………...

………………………………………………………………………………………………...

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

**Nakala safi**

………………………………………………………………………………………………...

………………………………………………………………………………………………...

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

**3. Matumizi ya Lugha** **(Alama 40)**

a) Andika maneno yenye vitamkwa vya sifa zifuatazo: (alama 2)

(i) kikwamizwa sighuna cha kaakaa gumu, irabu ya nyuma juu, kikwamizwa ghuna cha kaakaa laini, irabu ya nyuma juu, kilainisho na irabu ya mbele juu

……………………………………………………………………………………………….

FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

(ii) nazali ya midomoni, irabu ya mbele kati, nazali ya ufizini na irabu ya nyuma wastani

..………………………………………………………………………………………………….

b) Taja sifa zinazoonyesha usawa baina ya kila jozi ya sauti hizi. (alama 1)

(i) /m/ na /w/ ………………………………………………………………………………

(ii) /t/ na /ch/ ………………………………………………………………………………

c) Eleza maana **mbili** zilizo katika sentensi: (alama 2)

Usijadili mtihani unaoendelea wakati huu.

…………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

d) Tumia wingi kuandika sentensi zifuatazo.

(i) Mkulima alilima ucheu ili kujiandaa kwa msimu wa upanzi wa nafaka. (alama 1)

………………………………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………….

(ii) Shauri lake liliniepusha na janga la uwele hatari unaosambaa haraka. (alama 1)

………………………………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………….

e) Onyesha katika sentensi **moja** matumizi **mawili** ya ritifaa (‘) katika lugha. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

f) Zingatia maagizo katika mabano mwishoni mwa kila sentensi kuziandika upya.

(i) Wangia alipata mafunzo murua chuoni. Wangia ni stadi katika Kifaransa.

(Unganisha ukianzia: Mafunzo…) (alama 2)

………………………………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………….

(ii) <u>Sherehe</u> nyingi zilifanywa ili kuadhimisha <u>ushindi</u> wa Pute. (Tumia vitenzijina badala ya

FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

maneno yaliyopigiwa mistari.) (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(iii) Mari alinunua simutamba mpya kwa shilingi elfu kumi na kumtunza mwanafunzi bora.

(Anza na shamirisho ala.) (alama 2)

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

g) Ainisha mofimu katika maneno yafuatayo:

(i) katika (kitenzi) ………………………………………………………………... (alama 1)

(ii) achaguliwaye ………………………………………………………………… (alama 2)

h) Tunga mfano **mojamoja** wa sentensi kwa kila muundo.

(i) S - KN (Ɵ)+KT(Ts+T+H+N) (alama 1)

…………………………………………………………………………………………….

(ii) S - KN (W+V)+KT(t+N+V) (alama 2)

……………………………………………………………………………………………..

i) Bainisha kiima, kiarifu na chagizo katika sentensi hii. (alama 3)

Mhandisi shupavu atakagua ujenzi wa ghorofa hatua kwa hatua.

……………………………………………………………………………………………..

j) Eleza matumizi ya kiambishi **-o** katika sentensi ifuatayo: (alama 1)

Waliofanikiwa walifanya makadirio mazuri.

……………………………………………………………………………………………

k) Ainisha nomino katika sentensi hii: (alama 2)

Mashabiki wengi walipiga vigelegele Kocha Manoa alipowapa maji.

………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

l) Vishazi tegemezi vina dhima za kivumishi na kielezi. Tunga sentensi **mojamoja** kuonyesha kila dhima. (alama 2)

(i) kivumishi: ………………………………………………………………………………..

(ii) kielezi: ……………………………………………………………………………………..

m) Onyesha maana **mbili** za neno '**bunda**' kwa kutungia sentensi **mbili** tofauti. (alama 2)

(i) …………………………………………………………………………………………

(ii) …………………………………………………………………………………………

n) Kwa kutumia sentensi **moja**, onyesha miundo **miwili** ya virai husishi. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………….

…………………………………………………………………………………………….

o) Akifisha.

siku ya kiswahili duniani iliadhimishwa na wengi ilifana (alama 2)

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………….

p) Jaza mapengo kwa maneno yanayostahili. (alama 2)

Kinza ni kwa pinga na tambua ni kwa …………………………….. ilhali nata ni kwa ……………………………….

r) Onyesha katika sentensi maana ya nahau: '**shika shokoa**'. (alama 1)

…………………………………………………………………………………………..

s) Kasura aligundua kwamba Ogina alikuwa na uwezo mwingi wa kukabili Somo la Hisabati na akaamua kwenda mara kwa mara kupewa ushauri na Ogina hata akaimarika. Taja methali inayoweza kutumiwa kuafiki muktadha wa Kasura. (alama 1)

……………………………………………………………………………………………….

t) Kwa kuzingatia dhamira, sentensi ifuatayo inaweza kuwa katika **aina mbili**. Zitaje. (alama 1)

Mkiondoka wawiliwawili, mtafika haraka.

(i) ………………………………………………………………………………………………

(ii) …………………………………………………………………………………………….

**4. Isimujamii** **(Alama 10)**

a) Eleza sifa **tano** za lugha ambayo wewe kama mnyapara wa kiwanda cha kusaga miwa cha Kimatuni utatumia ukiwahutubia wafanyakazi walio chini yako. (alama 5)

……………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………….

b) *Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.* (alama 5)

"Polepole, Mama Mercy! Unajua si kupenda kwangu. Tena si hali itakayodumu milele. Baada ya siku chache tu, tutakuwa tumekamilisha mradi huo wenye dharura. Kisha tutakuwa na muda wa kila kitu. Hili, Mama Mercy, ni kile tunaita *bad coincidence*… nimebanwa na kazi. Unanielewa …?

“Dadii…njaa…sana!”

Fafanua sifa **tano** za lugha inayotumika katika huu muktadha wa familia. (alama 5)

……………………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………………….

FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

# SERIES 7 2023 MOCK

**(Hati ya kuhitimu Elimu ya Shule ya Sekondari Kenya- K.C.S.E)**

**102 / 2**

**Karatasi ya 2**

# KISWAHILI

## LUGHA

**Muda: Saa 2¹/₂**

---

**Jina: ……………………………….............................. …………  Nambari: ……………….…...**

**Shule: …………………………………………………………  INDEX………………..………..**

**TAREHE…………………………..SAHIHI…………………………LENGO………………...**

---

**MAAGIZO:**

a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasiulizoachiwa hapo juu.

b) Jibu maswali **yote**.

c) Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.

d) Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

e) Kijitabu hiki kina **kurasa 12** zilizopigwa chapa.

f) Kila mtahiniwa lazima ahakikishe kuwa **maswali yote yamo** na kuwa **kurasa zote**
. **chapa sawasawa**.

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE:**

FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM **0729125181**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| **1** | **15** | |
| **2** | **15** | |
| **3** | **40** | |
| **4** | **10** | |
| **Jumla** | **80** | |

**1. <u>UFAHAMU</u>: (Alama 15)**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.***

Zena alikuwa tayari ashayavulia nguo na alijua kuwa hana budi kuyaoga. Huu ulikuwa ni msimu wa kampeni za kumchagua mbunge wa eneo la Mtondo Kaskazini. Kwa mara ya kwanza tangu uhuru, mwanamke amejitolea kupigania kiti hicho. Hapo mjini tayari moto ulikuwa unawaka na midomo inatamba kuhusu hili.

Uchaguzi ulipokaribia Zena aliamua kuwaelezea wazazi wake nia yake. Siku moja baada ya chakula cha mchana, Zena aliwapasulia mbarika. Mamake, mdomo ulimfunguka lakini hakuwa na la kusema. Babake naye alitulia tulii kama maji mtungini. Baada ya muda, kama sasa wamepotokwa, mamake akaanza kusema,

"He! Hiyo kasheshe, huu ndio mwaka wa kuvuliwa nguo. Mtoto we! Hujatosheka? Umeona hutajwi tena midomoni unataka uanzwe tena kutafunwa kama ubani? Ridhika na umasikini."

"Baba nawe waonaje? Tumuache mama na mawazo yake?" Zena akamgeukia babake na kumuuliza,

Mzee Saidi alionekana kama yu mbali kimawazo. Alipoufungua mdomo alisema, "Mwanangu hilo ni ngumu! Umelifikiria vyema?"

Zena alimjuza babake kuwa alikuwa ameliwazia siku nyingi hata alipoamua.

"Basi, kama umelifikiri na ni uamuzi wako, ndilo ninalotaka kujua. Maana ulipotalikiana na mumeo Ali nilikuuliza vivyo na ukawa umeamua," Babake akaendelea, "Sitaki kukulazimisha na jambo. Ninakumbuka nilivyokukosea uliposema wataka kuendelea na masomo, nikasema hapakuwa na haja maadamu palikuwa na mume amesimama tayari kukuoa. Naomba msamaha."

Babake Zena aliuinamisha uso wake na kusema, "Ujuavyo ni kweli tumedanganywa sana. Tumepoteza nafasi ya kuuwajibisha uongozi kwa kuhongwa na kuuza kura zetu. Miaka mitano

iliyopita nilikuwa katika kundi letu la taarabu lililowapembeja raia wampigie mbunge wetu kura kwa kumwimbia nyimbo; ingawa alitimiza ahadi baadaye ya kuniajiri nimfanyie kazi shambani mwake, ilikuwa kwa muda mfupi tu wala sikupata mafao yoyote. Watu waaadilifu kama mamako wametamauka na hawataki siasa kamwe; anaamini kuwa wanasiasa wote ni sawa."

Zena hakuwa na wasimamizi wengi kama vile hakuwa na pesa za kulisha. Ni watu wa aila yake na marafiki wachache waliomuunga mkono. Alitayarisha mabango yake ya rangi nyeusi na nyeupe kwani vijipesa vyake havikutosha hata kufanya ya rangi. Mikutano ya hadhara ikaanza kuitishwa. Siku iliyofuata aliitisha mkutano katika uwanja wa Bajuri. Uwanja ulijaa tele na kufurika hata alipopanda jukwaani kuhutubu.

"Ndugu zangu wapenzi," alianza Zena, "Huu ni mwaka wa tano tangu tufanye uchaguzi uliompa mwenzangu kigoda. Katika kipindi hiki kumetokea mengi ya kujipiga kidari, pia **pametokea mengi ya kuitia jamii yetu ya Mtondo izara**. Tumejisuta kwa uteuzi usio wa kuridhidhisha ndio maana nimejitosa kwenye ulingo huu kuwaletea suluhu."

Kwa utaratibu na nadhari aliendelea, "Ndugu wapenzi, sina haja ya kuyafichua yote tuliyopitia; mmeyashuhudia yote. Malengo yetu ya kuwateua viongozi yamesalitiwa. Watangulizi wa Eneo la Mtondo walijitoa mhanga kupigana na maadui wetu watatu: Je, mnawajua maadui hao? Ni ujinga, magonjwa na umasikini. Waliowafuata walipigania huduma za bure za afya na elimu ya bure na ya lazima kwa wote. Vijana wetu walijitoma vyuoni kuzamia lulu ya elimu wakavidhihaki vitabu hadi kilelecha. La kusikitisha ni kuwa elimu hii imekuwa laana kwao. Mnajua kisa na maana ya hali hii? Natija iliyotarajiwa haikupatikana. Mnajua wapo vijana ambao wamepiga lami kwa miaka na mikaka bila kuambulia kazi walizoahidiwa huko vyuoni. Hatimaye hawa hawa wenye shahada mbili au tatu ndio wanaokuwa matarishi wa wale ambao walichechemea masomoni. Vijana wengine wameamua kuanzisha biashara rejareja ili kujikimu; Ukikosa la mama hata la mbwa huamwa. Sina haja ya kuwafafanulia kiini cha hali hii ya kutamausha."

Zena alitua na kumeza funda la mate, "Tumetendwa sote wenzangu, hebu niambie wewe mama mwenzangu, kuna faida gani kuuza kura yako kwa kibaba cha unga na noti ya shilingi mia moja? Je, faida imekuwa gani? Hujangojea kwa miaka mitano kusakafiwa kwa hiyo barabara uliyoahidiwa siku ulipouza kura yako? Na ile ahadi ya maji ya mabomba ilitokomea punde ulipopokea kibaba. Je, haiwaudhi kuwaona watu wa akraba moja wakisombwa kutoka humu kijijini kwenda kuchukua nyadhifa katika mashirika ya umma? Vijana wachache wa pangu pakavu wanapochukuliwa huenda kufanywa mawakala wa ulanguzi wa dawa za kulevya katika mahandaki jijini."

"Dau la masomo ya watoto wetu limeenda mrama huku tukimlilia huyo huyo mbunge Bwana Beka. Kila mara tunasikia kuwa serikali imeanzisha Hazina ya Eneobunge kuyafadhili masomo ya watoto masikini. Lengo kuu ni kuhakikisha kwamba asilimia kubwa ya watoto haipati fursa ya kujiunga na shule tu bali pia inakamilisha masomo. Mnione mimi hapa, nilikosa kuendeleza

FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

masomo kutokana na ukosefu wa karo, na usidhani ni karo ya shule ya kitaifa, la hasha! Ilikuwa shule ya kutwa. Isingekuwa Mola, ningekuwa windo rahisi la mmoja wa hao wabunge kama alivyofanywa maskini Rehema, bintiye Bi. Hamadi alipokosa karo na kusalia nyumbani ndipo akaambulia uja uzito ambao hakuulalia wala kuuamkia kwa ahadi ati angelipiwa karo," Zena alisimulia

Hata hotuba ya Zena ilipokamilika kwa kusema, "Ndugu zangu, hii ni awamu mpya, msimpe mtu mwenye mawaa kura!" alikuwa **amejikosha** kwelikweli. Bi. Cheusi ambaye alitega sikio ndi! tangu mwanzo alijiambia, "Huenda huyu atakuwa tofauti na wenzake. Vyema tumjaribu!"

a) Eleza mchango wa wanyonge katika hali ya uongozi wa eneo la Mtondo. (alama 4)

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………..

b) **"Pametokea mengi ya kuitia jamii yetu ya Mtondo izara."** Thibitisha ukweli
. wa kauli hii kwa kurejelea hoja **sita** kwenye taarifa hii. (alama 6)

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
……………………………………….....

c) Eleza mbinu **nne** ambazo Zena alitumia kuishawishi hadhira yake kumpigia kura
. kwenye taarifa hii. (alama 4)

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………….

d) Andika maana ya msamiati, "amejikosha" kama ulivyotumika katika taarifa hii. . (Alama 1)

…………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………

2. **UFUPISHO:** **(Alama 15)**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.***

Miili yetu hujengwa na chakula tulacho. Kila mara mwili wa mwanadamu hupoteza sehemu yake; kila kiungo kinapojimudu hutokwa na sehemu ndogo, na sehemu zile zinazotoka hurudishwa na chakula tulacho. Kila kiungo mwilini mwetu huhitaji sehemu fulani ya chakula.

Ubongo hauna budi kupata sehemu yake; mifupa, misuli na neva pia zinahitaji sehemu yao. Ni kazi ya ajabu sana inayobadilisha chakula kwa damu, na kutumia damu hii kwa kuvijenga viungo mbalimbali vya mwili; lakini kazi hii inaendelea daima, ikileta uzima na afya kwa kila neva, misuli na minofu hata kudhibiti mishipa, viwango vya sukari na mengine mengi.

Vyakula ambavyo vingechaguliwa kwa matumizi ni vile tu ambavyo vinahitajiwa kujenga mwili. Maana yake, si kwamba inatupasa kuchagua chakula kwa ajili ya utamu tu. Tamaa na ukosefu wa maarifa kuhusu aina za vyakula bora si mzuri. Imani ya watu wengi imepotoka kwa desturi mbaya za kula. Mara nyingi watu hutamani chakula hatari kwa afya kinachodhoofisha mwili na

kuleta udhaifu badala ya nguvu. Sio lazima tuongozwe na desturi za kikabila tunapoteua vyakula, baadhi ya imani zimepitwa na wakati na lazima zitupiliwe mbali. Maradhi mengi na maumivu yanayoenea pote duniani kama presha, kisukari, saratani na uzito uliokithiri hutokana na makosa ya wanadamu katika kuchagua chakula.

Nafaka, matunda, kokwa na mboga ndivyo vyakula tulivyochaguliwa na Muumba wetu. Vyakula hivi, vikiandaliwa vyema, vinaleta afya mwilini na kututia nguvu. Vinamtia mwanadamu nguvu, uwezo wa kuishi miaka mingi na akili timamu ambazo hazipatikani katika vyakula vilivyoungwa sana.

Lakini si kwamba vyakula vyote tunavyokula vinafaa mahitaji yetu katika hali zote. Ingetupasa kujihadhari sana katika kuchagua vyakula. Chakula chetu kingefuatana na hali ya majira, hali ya nchi tunapokaa, pamoja na kazi tunayoifanya. Vyakula vingine ambavyo vinaweza kutumiwa katika majira fulani ya mwaka na katika hali fulani ya nchi havifai kutumiwa kwa hali ya nchi nyingine, na katika majira mengine. Hivyo basi ni bora watu wawe na maarifa haya na mengine ya kuwaongoza. Hivyo basi kuna vyakula maalum vinavyofaa kwa watu wanaofanya kazi ngumu za juhudi na havifai kutumiwa na watu wanaofanya kazi za afisini, na inampasa kila mtu achague namna ya vyakula ambavyo kwa ujuzi wake ameviona kuwa vinafaa kwa mahitaji yake.

Maswali:

a) Bila kupoteza maana, fupisha mawazo makuu katika aya tatu za kwanza za taarifa hii
. kwa maneno (65-70) (alama 8)

Nakala chafu

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………

Nakala safi

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………

b) Fupisha aya mbili za mwisho za taarifa hii kwa (maneno 60-65)

. (Alama 6, mtiririko alama 1)

Nakala chafu

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
………………………………………

Nakala safi

……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
………………………………………

**3. MATUMIZI YA LUGHA:** (Alama 40)

a) (i) Andika kitamkwa chenye sifa zifuatazo. (alama 1)

Vokali ya mbele, wastani ……………………………………………

(ii) Andika neno lenye muundo ufuatao: (alama 1)

Konsonanti + konsonati, irabu + konsonanti, konsonati, irabu

…………………………………………………………………………………………………..

b) Neno "*bao*" lina maana ya pande pana la mti lililochongwa pia ni goli katika mchezo.

. Andika sentensi kubainisha maana nyingine ya neno hilo. (alama 1)

……………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………….

c) (i) Eleza maana ya "*mofimu*". (alama 1)

……………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………….

(ii) Andika kwa kutolea mfano, dhima **mbili** tofauti za mofimu "**O**" katika

. maneno ya Kiswahili. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..…

d) (i) Eleza maana ya "*sentensi hisishi*" (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………..

(ii) Eleza aina ya sentensi ifuatayo *kuzingatia dhamira*. (alama 1)

Funga majani matano matano kwa kila fungu.

…………………………………………………………………………………………………..

e) (i) Andika sentensi fupi kubainisha *kitenzi kishirikishi kikamilifu*. (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………..

(ii) Andika sentensi ifuatayo upya *bila kutumia vitenzi visaidizi*. (alama 1)

Wachezaji huenda wakawa wanaweza kushinda mchezo wa leo.

…………………………………………………………………………………………………..

f) Ainisha *vihusishi* katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

Mgeni aliwasili mapema kuliko wenyeji halafu akaondoka.

FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

…………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………….

g) Andika sentensi zifuatao upya kulingana na maagizo uliyopewa kwenye mabano baada ya kila moja. (alama 3)

(i) Makuli hawajawaarifu mbao hazikuwa zetu? *(umoja)*

……………………………………………………………………………………………......

(ii) Badi huwa hapitii hapa, huenda usimpate. *(yakinisha)*

………………………………………………………………………………………………..

(iii) Mtoto alikusanya vitu vyake kabla ya kukoga. *(kinyume)*

………………………………………………………………………………………………..

h) (i) Andika sentensi fupi ukitumia *kiunganishi cha majuto*. (alama 1)

………………………………………………………………………………………………

(ii) Andika sentensi hizi upya kama sentensi moja *bila kutumia kiunganishi* kuonyesha kutegemeana. (alama 1)

Mahakama ilitatua mzozo. Kulikuwa na majaji waadilifu.

…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

i) Andika kwa kutolea mfano, matumizi mawili ya alama ya uakifishaji ya *semi koloni* **;** (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………….

j) (i) Andika sentensi ifuatayo upya katika *hali ya mazoea* bila kutumia "*amba-*"
. rejeshi. (alama 1)

Mti ambao ulivunjika uliperushwa na tufani.

……………………………………………………………………………………………..

(ii) Andika sentensi ifuatayo upya katika *wakati ujao hali ya mazoea.* (alama 1)

Uchaguzi hufanywa baada ya miaka mitano.

……………………………………………………………………………………………..

k) Andika kifungu kifuatacho upya kama usemi halisi. (alama 2)
. Mwajiri wangu alitaka kujua kwa mshangao nilivyoweza kuubeba mzigo huo pekee
. yangu siku hiyo.

…………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

l) (i) Andika nomino moja kutokana na kitenzi: "*Kinai*" (alama 1)

……………………………………………………………………………………………..

(ii) Andika sentensi ifuatayo upya kwa kubadili vitenzi vilivyopigiwa mstari kuwa
. nomino. (alama 1)
. Jangwa <u>linaenea</u> kwa sababu watu <u>wanaharibu</u> misitu.

……………………………………………………………………………………………..

m) (i) Eleza maana ya : "*Kirai*". (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………..

(ii) Changanua sentensi ifuatayo kwa *kielelezo cha mstari*. (alama 1)

Mtoto wa mwalimu wetu ni mwadilifu.

……………………………………………………………………………………………..

n) Andika sentensi kubainisha matumizi yafuatayo ya kiambishi maalum "*ji*" (alama 2)

(i) Unominishi

…………………………………………………………………………………………………

(ii) Urejeshi

…………………………………………………………………………………………………

o) (i) Eleza maana ya : "*kishazi*". (alama 1)

……………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………..................

(ii) Andika sentensi ukitumia *kishazi kitegemezi* kama *kivumishi*. (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………

p) Andika sentensi *kwa kila moja* ili kutofautisha vitate vifuatavyo kimaana. (alama 2)

(i) Kasa

……………………………………………………………………………………………..

(ii) Kaza

……………………………………………………………………………………….........

q) (i) Andika sentensi ukitumkia *kiwakilishi cha pekee* cha *ujumuishi.* (alama 1)

……………………………………………………………………………………………..

(ii) Andika sentensi ukitumia *kiwakilishi kisisitizi cha karibu* cha ngeli ya LI-YA.
. (alama 1)

……………………………………………………………………………………………..

r) Andika sentensi zifuatao upya kulingana na maagizo uliyopewa kwenye mabano
. baada ya kila moja. (alama 2)

. (i) Msasi alimnywesha mbwa maziwa kwa kigae. *(Anza kwa yambwa tendewa)*

……………………………………………………………………………………………..

(ii) Seremala alinyosha mbao. Seremala alikuwa kiwandani. *(Anza: Kiwandani...)*

……………………………………………………………………………………………..

s) Andika maana mbili tofauti zinazoibuliwa na sentensi ifuatayo. (alama 2)

Wageni hawaogopi baridi kama wenyeji.

…………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

t) Andika semi moja inayoafiki maelezo yafuatayo. (alama 1)

Si vyema kumzuia mtu kufaidi na kitu ilhali binafsi haukitumii au kufaidi nacho.

……………………………………………………………………………………………………

**4.** **ISIMUJAMII**: (Alama 10)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

***"…Kwa mujibu wa ushahidi uliotolewa, imethibitishwa kwa uwazi kwamba Mshtakiwa wewe, Badi Guyo ulihusika katika udukuzi wa mtandao wa tume ya IEBC usiku wa Agosti tarehe 9, 2022 baina ya saa tano na saa kumi na moja alfajiri na kubadili fomu halisi za Urais zilizotumwa humo …Unahukumiwa kwa uhaini."***

a) Andika ithibati **sita** kwenye makala kuonyesha ni sajili ya kisheria. (alama 6)

…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
………………………………………

b) Fafanua sifa nyingine **tatu** za lugha ya kisheria ambazo zingejitokeza katika makala
. haya. (alama 3)

…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………….

c) Eleza maana ya msamiati "*uhaini*" kama unavyotumika katika sajili hii. (alama 1)

……………………………………………………………………………………………………..

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.**

---

**102/2 - KISWAHILI**
**KIDATO CHA NNE 2022**

# SERIES 8 2023 MOCK

**Ufahamu, ufupisho, Sarufi na matumizi ya lugha na Isimu jamii**
**MUDA SAA 2 ½**

---

**JINA:........................................................................ ………….. Nambari ya usajili:…………..**

**SHULE………………………………………………………..INDEX………………………..**

**Tarehe …………………………SAHIHI……………………..LENGO………………………..**

**MAAGIZO**

*v) Andika jina na nambari yako kwenye nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
*vi) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani.*
*vii) Jibu maswali yote.*
*viii) Andika majibu yako katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
*ix) Majibu yako yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | ALAMA | TUZO |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| JUMLA | 80 | |
| | | |

FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

## c) UFAHAMU

Katiba ni utaratibu wa sharia unaoweka mpango wa jamii kuendesha mambo.Ni muhimu kila raia ajue katiba ya nchi yake.

Katibu yaweza kuwa imeandikwa au haikuandikwa .Katika jamii za jadi,katiba ilihifadhiwa na kupokezwa kwa mdomo. Mtindo wa kuandika katiba ulianza nchini Marekani mwaka 1787.Ingawa katiba hii imefanyiwa mabadiliko hapa na pale,bado ni ili ile .Kenya ilipowekwa chini ya himaya ya Uingereza mwaka 1895,ilianza kutumia katiba ya Uingereza. Baada ya masetla wa kikoloni kujikita,walitangaza Kenya kuwa koloni.Hii ililazimu pawe na katiba nyingine mwaka 1920.Waafrika waliupinga mfumo huu kwa sababu haukuwahusisha kikamilifu kwenye masuala ya uongozi.Utetezi wa wanasiasa uliilazimisha serikali ya Uingeza kuitisha makongamano mbalimbali kama vile lile la Devonshire na mengine ili kurekabisha katiba.Waafrika hawakuridhika .Wakaendelea kudai katiba mwafaka.Harakati hizi zilileta kuitishwa kwa kongomano la katiba la Lanchester.Lengo lilikuwa kuandika katiba itakayotumiwa nchini hadi leo.Kati ya wajumbe walioenda Uingereza kuandika katiba mwaka 1962 ni pamoja na Tom Mboya ,,Jean Marie Seronney,Julius Kiano,Jomo Kenyatta,Masinde Mulio,Oginga Odinga,Ronald Ngala,Daniel Arap Moi na James Gichuru.Wengine ni Martin Shikuku,Dennis Akumu,Taita Towett,Abdilahi Nasssi,Jeremiah Nyaga na John Keen.

Katiba ni kitovu cha taifa.Baina ya mambo inayotokeleza ni kuweka utaratibu na kanuni za utawala,kwa mfano,utawala wa kimikoa na serikali za wilaya.Pamoja na haya ,katiba hufafanua vyombo vikuu vya serikali,mamlaka yavyo na mipaka yavyo ya kutenda.vyombo hivi ni bunge,mahakama,urais,jeshi n.k.Halikadhalika,katiba hupambanua haki za raia.

Hii hudumisha demokrasia na huwawezesha wananchio kupata uhuru na haki za kimsingi.Katiba hukinga haki za kila raia,hasa kutokana na udhalimu na wengi au wenye uwezo mkubwa .Zaidi ya yote,katiba huimarisha asasi za umma ili kudumisha uwajibikaji.

Katiba huhalalishwa na watawaliwa.Hii hutokea wanaposhirikishwa katika uandishi wake.Kuanzia miaka ya themanini ,RAIA WALIANZA KUDAI KATIBA IGEUZWE.mwamko wa kutaka mageuzi ulianza kwa harakati za kibadilisha mfumo wa kisiasa kutoka ulee wa chama kimoja hadi ule wa demokrasia ya vyama vingi.Haja ya mfumo mpya wa kisiasa kutoka ule wa chama kimoja hadi ule wa demokrasia ya vyama vingi.Haja ya mfumo mpya wa kisiasa ulilenga kuwashirikisha wananchi katika utawala na kuondoa uimla.

Harakati zilitia fora miaka ya tisini.Mambo yaliyochochea hali hii ni mengi.Kwanza katiba iliyokuwa imeandikwa na watu wachache ilikuwa imefanyiwa marekebisho mengi.Marekebisho haya yalimpa rais mamlaka mengi juu ya serikali kuu na vyombo tofauti vya serikali.Pili,viongozi na watu wenye uwezo na utajiri walipuuza katiba.Raia walihisi wanadhulumiwa .Walipinga hali ya wachache waliomzunguka rais kunufaika huku umma ukitengwa.Tatu,kutokana na uongozi uliokuweko wakati huo,wanawake,Watoto na walemavu walidhulumiwa na kukosa uwakilishi ufaao.Hatimaye,pakawa na ongezeko la uharibifu wa mazingira,ufisadi na unyakuzi wa mali ya umma kama vile ardhi.

Waliopigania katibu mpya walikuwa na haja ya katiba ambayo uanddikaji wake ungewahusisha Wakenya wote.Mwanzoni,serikali ilipinga mwito wa madiliko.Lakini mnamo mwaka 2001 iliunda Tume ya marekebisho ya katiba ili kutekeleza mahitaji ya wananchi.Tume hii iliwahamasisha na kuwashawishi raia kutoa maoni.Tume iliandaa vikao katika maeneo ya ubunge 210 ambapo wananchi walitoa mapendekezo kuhusu marekebisho ya katiba.

Katika mapenekezo hayo raia walisisitiza mambo kadha.Jambo la kwanza ni utawala mwema na uwajibikaji wa viongozi na maafisa wa wa umma .Jambo linguine ni kulinda haki za binadamu zikiwemo za wanawake,Watoto na walemavu .Raia walidai kanuni za usawa na ulinganifu.Aidha walitia mkazo mahitaji ya msingi kama chakula,afya nzuri,makao,elimu,usalama,uchumi na kadhalika.

Msingi wa mapendekezo haya yote ni kuwepo na amani ya kitaifa,umoja na uadilifdu ili kulinda maslahi ya wananchi wote na taifa.

Maswali

5. Eleza kilichosababisha kongamano la Lancaster. (alama 3)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

6. Taja mambo matatu yaliyotiliwa mkazo na raia katika maonoi yao kuhusu katika. (alama 3)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

7. Eleza umuhimu wa katiba kwa mujibu nwa taarifa. (alama 3)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

8. Taja sababu zilizochangia ubadilishaji wa katiba. (alama 3)

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

9. Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika taarifa. (alama 3)
   iii) Kitovu

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

   iv) Harakati

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

   v) Hamasisha

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

## d) UFUPISHO

